**East African Journal of Swahili Studies**
eajss.eanso.org
**Volume 7, Issue 1, 2024**
**Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475**
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili

*Priscah Katunge Lucas[1*] na Leonard Chacha Mwita, PhD[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Kenyatta, S.L.P 43844-00100 Nairobi, Kenya.
[*] ORCID ID: https://orcid.org/0000-0003-3432-1331; Barua pepe ya mawasiliano: priscahlucas1@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*31 Oktoba 2024*

**Istilahi Muhimu**:

*Viambajengo Katizwa, Sentensi Katizwa, Virai Katizwa.*

## IKISIRI

Makala hii inachunguza udhihirikaji wa viambajengo katizwa katika Kiswahili. Viambajengo katizwa ni elementi za neno au kishazi ambazo hazipatikani katika usanjari mmoja kwa sababu elementi kutoka mofu au kirai kingine zimeingilia kati (Reinholtz, 1999). Hili hutokea wakati mofu kadhaa za kiambajengo kimoja zimetengwa au maneno kadhaa ya kirai kimoja yametengwa. Kwa mfano: "Rais alizungumza, bila shaka, juu ya siasa." Katika sentensi hii, kitenzi na kielezi chake vilitengwa na taarifa nyingine. Nadharia ya Sarufi Miundo Virai Katizwa iliyozungumziwa na Harman (1963) iliongoza utafiti huu. Data ya makala hii ilikusanywa nyanjani ambapo wataalamu wa lugha ya Kiswahili walihojiwa kuhusu usahihi wa sentensi katizwa na hata kusaidia kuzalisha zingine. Mbinu ya usampulishaji wa kimaksudi ilitumika katika uteuzi wa sampuli. Data ya utafiti huu ilibaini aina mbili kuu za virai katizwa. Ilibainika kuwa viambajengo katizwa husababishwa na ukanushi wa baadhi ya vitenzi, ukanushi maradufu, njeo vishazi tegemezi na vishazi viongezi. Tafiti zingine zinaweza kufanywa kuhusu udhihirikaji wa viambajengo katizwa katika aina nyingine ya kirai kama vile kirai kihusishi au kirai kivumishi katika lugha ya Kiswahili au lugha nyingine.

**APA CITATION**

Lucas, P. K. & Mwita, L. C. (2024). Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili. *East African Journal of Swahili Studies*, *7*(1), 514-524. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355.

**CHICAGO CITATION**

Lucas, Priscah Katunge and Leonard Chacha Mwita. 2024. "Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies* 7 (1), 514-524. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

**HARVARD CITATION**

Lucas, P. K. & Mwita, L. C. (2024) "Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili", *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), pp. 514-524. doi: 10.37284/jammk.7.1.2355

**IEEE CITATION**

P. K. Lucas, & L. C. Mwita "Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili", *EAJSS*, vol. 7, no. 1, pp. 514-524, Oct. 2024.

**MLA CITATION**

Lucas, Priscah Katunge & Leonard Chacha Mwita. "Udhihirikaji wa Viambajengo Katizwa Katika Lugha ya Kiswahili". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 7, no. 1, Oct. 2024, pp. 514-524, doi:10.37284/jammk.7.1.2355.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

## UTANGULIZI

Kwa kawaida lugha huwa na vipashio vinavyofululiza vikifuata kanuni husika ili kuzua maana. Vipashio vinapokosa kufululiza inavyohitajika katika lugha huleta utata na kukosa kukubalika lakini inatokea kwamba vipashio vichache visivyofululiza katika lugha bado hukubalika na kutoa maana. Kiswahili ni lugha yenye muundo wa maneno usiobadilika na hivyo itaruhusu sentensi chache ambazo ni katizwa. Pia, aina ya sentensi katizwa katika lugha moja huwa tofauti na zile za lugha nyingine ijapokuwa kuna uhusiano wa karibu. Kwa hivyo, makala hii itakuwa chanzo cha msukumo katika kutambua masuala anuwai kuhusu viambajengo katizwa katika lugha ya Kiswahili. Kwa kufanya hivi, taaluma ya isimu itapanuliwa kiusomi na kupanua maarifa kuhusu usarufi wa viambajengo katizwa katika lugha ya Kiswahili. Makala hii imegawanywa katika sehemu zifuatazo; utangulizi, maelezo kuhusu dhana za viambajengo katizwa, sentensi katizwa na virai katizwa, nadharia, mbinu za utafiti, uchanganuzi wa sentensi katizwa na virai katizwa katika Kiswahili na hitimisho.

## Dhana za viambajengo katizwa, mofimu katizwa, sentensi katizwa na virai katizwa

Sehemu hii inatoa ufafanuzi wa dhana ambazo ni za kimsingi na zitakazosaidia katika uelewaji wa makala hii. Reinholtz (1999) anaeleza viambajengo katizwa kama elementi za neno au kishazi ambazo hazipatikani katika usanjari mmoja kwa sababu elementi kutoka mofu au kirai kingine zimeingilia kati. Naye Massamba (2004) anaeleza mofimu katizwa kuwa mofimu ambayo inaanza na kisha ikaingiliwa kati na mofimu nyingine na baada ya hapo ikaendelea. Massamba (2004) anafafanua sentensi katizwa kama sentensi ambayo kabla ya kumalizika kwake huchopekwa neno au tungo nyingine ndipo ikaendelea ilhali Kirai katizwa, kwa mujibu wa utafiti huu, ni kirai ambacho kinaingiliwa kati na neno au tungo nyingine kisha kinaendelea.

## Nadharia


Nadharia iliyoongoza utafiti huu ni nadharia ya sarufi miundo virai katizwa. Nadharia hiyo iliasisiwa na Harman (1963). Historia ya sarufi miundo virai katizwa imefungamana na historia ya sarufi muundo virai. Manaster-Ramer & Kac (1990) wanaeleza kwamba dhana ya muundo kirai ilianza pale ambapo Bloomfield (1933) alieleza kwamba muundo wa kisintaksia wa sentensi uliweza kuelezwa kikamilifu kwa kuuchanganua katika viambajengo vifuasi na kuendelea kuchanganua kila moja hadi kufikia viambajengo tamati (yaani mofimu). Harman (1963) alijaribu kupanua nadharia hii ya Chomsky ili ishughulikie viambajengo katizwa inayozungumzia sheria za uandikaji upya zinazoeleza miundo katizwa. Kulingana na Harman (1963), nadharia ya sarufi miundo katizwa ina misingi ifuatayo:

### Dhana ya mchoroti katizwa.

Huu ni muundo wa mfano wa mti unaoeleza viambajengo katizwa na ni jambo la kimsingi katika nadharia hii. Mhimili huu ulitumika kuchanganua viambajengo katizwa katika kiwango cha sentensi.

### Kanuni muundo virai huweza kutumiwa kuwakilisha miundo katizwa.

Kanuni muundo kirai huandika upya kiambajengo kuwa mfululizo wa viambajengo jozi vilivyopakana. Kwa hiyo, uundaji wa kanuni muundo kirai katika michoroti katizwa huhitaji dhana ya kupakana katika miundo hiyo. Ukiwa na muundo kama huu ulio hapa chini unaweza kutunga kanuni muundo kirai.




Kanuni muundo kirai sahihi ya kuzalisha muundo wa sentensi ulio hapo juu ni S $\rightarrow$ A + B + [Y] + C ambapo mabano ya mraba yanaonesha kwamba Y haitawaliwi na kifundo S, lakini ni muktadha wa ndani tu. Mfululizo ulio kwenye kanuni hii una

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

matatizo kwa kuwa nafasi ya Y haibainiki waziwazi. Ili kutatua tatizo hilo, dhana ya mfuatano wa kupakana ilizungumziwa.

**Dhana ya tatu muhimu ni mfululizo wa mfuatano wa kupakana.**

Dhana hii hutoa maelezo ya jumla kuhusu dhana ya jozi inayopakana au ujirani wa kushoto na kulia kama inavyotokea katika miundo yenye ukatizwaji. Dhana hii huwezesha utungaji wa kanuni za uandikaji upya ambazo zinaeleza miundo katizwa kama ilivyo katika kanuni muundo kirai $S \rightarrow A + B + [Y] + C$, ambapo ishara + inawakilisha mfuatano wa kupakana. Katika sentensi hii ni wazi kwamba A inapakana na B, na B inapakana na C. Mhimili huu ulitumika kueleza uhusiano wa vipashio vya miundo katizwa vilivyopatikana na vile vilivyoleta ukatizwaji.

**Ukosefu wa uchomozi**

Uchomozi ni kanuni ya michoroti ambayo kwayo ukatizwaji unaweza kutambuliwa na kuelezwa. Mchoroti husemekana kwamba una uchomozi ikiwa hakuna mistari inayokingama. Ikiwa kuna mistari inayokingama basi muundo uliopo hauna uchomozi na hivyo unakiuka uchomozi kwa namna moja au nyingine.

**Uteuzi wa sampuli na ukusanyaji wa data**

Usampulishaji kimaksudi ulitumiwa kuteua mofimu katizwa kumi na tano, virai katizwa kumi na tano, sentensi katizwa ishirini na tano za Kiswahili kutokana na mahojiano na wahadhiri wa Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Kenyatta na pia kutoka kwa vitabu vya sarufi ya Kiswahili vilizo na dhana ya ukatizwaji. Sababu kuu ya kuteua sampuli hii ni kutokana na kuongozwa na maoni ya Milroy (1987) ambaye anapendekeza matumizi ya sampuli ndogo katika uchunguzi wa lugha kwa kuwa sampuli kubwa inaweza kuzua data yenye urudufu mwingi. Uteuzi wa kimaksudi uliwezesha wataalamu kujibu maswali ya mahojiano na kutupatia matokeo faafu. Mahojiano yenyewe yalihusisha walengwa kumi na mahojiano yalikuwa ya ana kwa ana ambapo kila mtaalamu alihojiwa kivyake. Hii ni kutokana na maelezo ya Lincoln na Guba (1985) kuwa idadi ya wahojiwa kuanzia kumi hadi ishirini itafaa katika utafiti wa maelezo. Walengwa wengi hawakuhitajika kwa sababu ya vigezo ambavyo vilizingatiwa.

## UCHANGANUZI WA VIAMBAJENGO KATIZWA KATIKA KIWANGO CHA VIRAI NA SENTENSI

Sehemu hii ilichunguza uchanganuzi wa viambajengo katizwa katika kiwango cha virai katizwa na sentensi katizwa kwa mujibu wa nadharia ya sarufi miundo virai katizwa.

**Miundo ya Virai katizwa**

Chomsky (1965) alitambua kuwa sentensi huundwa na miundo mbalimbali ya viambajengo. Miundo ya viambajengo hivi ni pamoja na; kategoria virai na kategoria leksia. Istilahi kama vile kirai nomino, kirai kitenzi, kirai kihusishi ni mojawapo ya viambajengo vya kategoria virai. Kategoria leksia ilihusisha istilahi za isimu zifuatazo; nomino, kitenzi, kivumishi, kielezi, kiwakilishi, kihusishi, kiunganishi na kihisishi. Kirai ni kipashio cha kimuundo chenye neno tawala kinachotokana na muungano wa kategoria za maneno (Poole, 2002; Massamba, 2004; Habwe na Karanja, 2004). Kirai katizwa, kwa mujibu wa utafiti huu, ni kirai ambacho kinaingiliwa kati na neno au tungo nyingine kisha kinaendelea. Kwa mfano, kirai kitenzi kinaweza kikachopekwa kiunganishi, kielezi, neno au tungo kabla ya kukamilika kwake na kisha kikaendelea. Kutokana na utafiti huu, tulibaini aina mbili za virai katizwa ambazo ni kirai kitenzi katizwa na kirai nomino katizwa.

**Kirai kitenzi katizwa**

Rubanza (2003) anaeleza kuwa kirai kitenzi ndio msingi mkuu wa sentensi katika lugha ya Kiswahili. Kutokana na utafiti huu, kirai kitenzi katizwa ni mifano inayohusu nahau ambazo zinaweza kutenganishwa katika sentensi kwa kupachika kipashio kingine bila ya kupoteza maana yake asilia. Kirai kitenzi katizwa huwa ni kipashio katika sentensi ambacho kinabeba kitenzi kikuu cha sentensi. Utafiti huu ulichunguza muundo wa kirai kitenzi (KT) katika

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

lugha ya Kiswahili ambapo mtafiti alibainisha vipashio vinavyoandamana na kitenzi (T) katika sentensi kwa mujibu wa nadharia ya sarufi miundo virai katizwa yake Harman (1963).

**Mifano ya virai vitenzi katizwa**


Utafiti huu ulibaini mifano ifuatayo ya virai vitenzi katizwa tuliyoichanganua kwa njia ya matawi kwa kuzingatia michoroti katizwa kwa mujibu wa nadharia ya sarufi miundo virai katizwa.

1. Mzee huyu **amekula** kwa kweli **chumvi nyingi**
2. Juma **alifunga** juzi **pingu za maisha**.
3. **Amekuwa** kwa hakika **popo**.
4. Mambo ya shule **yamemwendea** mwanafunzi yule **mrama.**
5. Kamau pamoja na Juma **walikula** juzi **njama** juu ya rafiki yake.
6. Babu **anafuta** mara nyingi **mawazo.**
7. Maria **alijipa** sana **moyo.**
8. Bunge **lilipiga** mawaziri **darubini** jana asubuhi.

Mifano hii iliweza kuchanganuliwa kwa njia mbalimbali kama inavyojidhihirisha hapa chini;

1. Mzee huyu **amekula** kwa kweli **chumvi nyingi**

Katika mfano huu, kirai kitenzi katizwa ni ‘amekula kwa kweli chumvi nyingi’ na mfano huu wa kirai kitenzi katizwa uliweza kuchanganuliwa kwa njia ya mchoroti katizwa kama inavyojidhihirisha hapa chini.





Katika mfano huu, nahau ‘kula chumvi nyingi’ inamaanisha kuishi miaka mingi lakini katika sentensi hiyo, mfululizo wake wa kawaida umekatizwa na uchopeakaji wa kihusishi ‘kwa kweli’ na kuifanya kuwa kirai kitenzi katizwa ‘amekula kwa kweli chumvi nyingi.’ Kwa kawaida, nahau huwa na umbo sawa na virai vya kawaida isipokuwa huwa zimeganda katika umbo lake kiasi kwamba huwezi kubadili hilo umbo kwa urahisi au mpangilio wake wa maneno. Hata hivyo, utafiti huu ulibaini kuwa nahau zinaweza pia zikakiuka kanuni hizi za kisemantiki na kusababisha kuwepo kwa ukatizwaji.

2. Juma **alifunga** juzi **pingu za maisha**.

Kutokana na mfano huu wa kirai kitenzi katizwa, tuliwasilisha dhana ya mchoroti katizwa kama inavyoashiriwa hapa chini.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355




Utafiti huu ulibaini ya kwamba, sentensi iliopo hapo juu ina kirai kitenzi katizwa. Nahau 'funga pingu za maisha' imetenganishwa na kielezi 'juzi' na kinachokatisha mfululizo wa maneno hayo na kuwa 'Juma alifunga juzi pingu za maisha' na hivyo basi kuifanya kuwa kirai kitenzi katizwa.

Kutokana na mfano huu, kirai kitenzi katizwa ni 'alifunga pingu juzi za maisha' ambacho hakifululizi bali kimekatizwa na kielezi 'juzi'. Mchoroti huu uliweza kuelezwa kuwa na ukosefu wa uchomozi. Uchomozi, kulingana na Harman (1963), ni kanuni ya michoroti ambayo kwayo ukatizwaji unaweza kutambulika na kuelezwa na mchoroti husemekana huna uchomozi ikiwa kuna mistari inayokingama. Mfano uliopo hapo juu una mistari inayokingama na kwa hivyo ukatizwaji uliweza kutambulika.

3. **Amekuwa** kwa hakika **popo**.

Katika mfano huu, nahau 'amekuwa popo' ina maana ya kutoeleweka au kuwa kigeugeu. Nahau hii imeingiliwa kati na kiunganishi cha kuonyesha matokeo 'kwa hakika' katika sentensi na kuifanya kutofululiza inavyostahili na kuwa kirai kitenzi katizwa 'amekuwa kwa hakika popo' japo inaleta maana inayokusudiwa. Tuliweza kuchanganua mfano huu kwa njia ya mishale;

S → KT +[KU]+ KN

KT → T

T → Amekuwa

KU → U

U → Kwa hakika

KN → N

N → popo


Kutokana na kanuni hii ya mshale, mabano ya mraba yanaashiria kwamba kirai kiunganishi [KU] hakitawaliwi na kifundo S, bali ni mukatadha wa ndani tu. Kwa hivyo, kutokana na mfano huu ni wazi kwamba kirai kitenzi katizwa ni 'amekuwa kwa hakika popo.'

**4.** Mambo ya shule **yamemwendea** mwanafunzi yule **mrama.**


Mfano huu ulichanganuliwa na kuwasilisha kwa njia ya mchoroti kama inavyodhihirika hapa chini.

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355




Kutokana na utafiti huu, maneno ‘yamemwendea mwanafunzi yule mrama’ katika sentensi hii, yanaashiria kuwepo kwa kirai kitenzi katizwa. Ukatizwaji huu ulidhihirika kutokana na uchopekaji wa kirai nomino ‘mwanafunzi yule’ uliokatiza mfululizo wa nahau ‘kwenda mrama’ iliyo na maana ya kuharibika bila ya kupoteza maana iliyokusudiwa katika sentensi hiyo. Tuliweza kuuchanganua mfano huu kwa njia tofauti kuonyesha ukatizwaji wa kirai kitenzi katizwa kama ifuatavyo:





Kulingana na mchoroti huu, kirai kitenzi katizwa ni ‘yamemwendea mwanafunzi yule mrama’ na kwa kawaida ‘enda mrama’ ni maneno ambayo yanayopaswa kuwa pamoja ilhali yamekatizwa na kirai nomino ‘mwanafunzi yule’, jambo lililosababisha kuwepo na mstari wa ukingamo.

Kutokana na uchanganuzi uliofanywa, ni wazi kuwa mifano ya virai vitenzi katizwa nambari tano hadi nane hapo juu vinaweza pia kuchanganuliwa kwa njia hiyo hiyo ya mchoroti katizwa ilivyo katika mfano wa kwanza hadi wa nne. Mifano hiyo inaashiria virai vitenzi katizwa kwa sababu nahau zilizotumika katika sentensi hizo zimekatizwa ufululizaji wake kwa uchopekaji wa tungo mbalimbali.

**Kirai nomino katizwa**

Utafiti huu ulibaini kirai nomino katizwa kuwa aina mojawapo ya kirai katizwa. Kirai nomino katizwa ni nahau ambazo neno lake kuu ni nomino lakini kabla ya kumalizika kwake kuna uchopekaji wa neno au tungo nyingine ndipo ikaendelea. Utafiti huu ulibaini na kuchanganua mifano ya virai nomino katizwa iliyopo hapo chini.


**Mfano wa 1**: Mwanabiashara huyu ana **ulimi** lakini **wa upanga**. Mfano huu ulichanganuliwa kwa njia ya mchoroti katizwa kama inavyoonyeshwa hapa chini.




This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.


Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

Mfano huu unadhihirisha kirai nomino katizwa ambacho ni ‘ulimi lakini wa upanga’ na ambacho kimekatizwa ufululizaji wake na kiunganishi cha kuonyesha kinyume cha matarajio ‘lakini’. Tuliweza kuchanganua mfano huu kwa njia tofauti kama;





**Mfano wa pili**: Mtoto yule ana **mkono** ila **wa birika.**

Sentensi hii imeundwa na nahau ‘mkono wa birika’ iliyo na maana ya mtu mchoyo na kirai nomino katizwa ‘mkono ila wa birika’ na hii ni kwa sababu kiunganishi cha kuonyesha kinyume cha matarajio ‘ila’ kimeingilia kati na kukatiza mfululizo wa nahau hiyo. Kwa hivyo, uchanganuzi wa mfano huu ni kama inavyobainishwa hapa;




Kutokana na mfano huu, kirai kiunganishi kimetengwa kutoka kwa kichwa chake na elementi inayotawala kichwa chake na hivyo basi kusababisha kuwepo na ukatizwaji.

Mfano huu wa kirai nomino katizwa uliweza kuchanganuliwa kwa namna tofauti kama inavyojidhihirisha hapa chini;




Kwa mujibu wa kanuni KN $\rightarrow$ N + [U] + KH ni wazi kwamba kiunganishi ‘ila’ kimekatiza mfululizo wa nahau na uufanya katizwa.

**Sentensi katizwa**

Kulingana na Massamba (2004), sentensi katizwa ni sentensi ambayo kabla ya kumalizika kwake huchopekwa neno au tungo nyingine ndipo ikaendelea. Kutokana na utafiti huu, sentensi katizwa za lugha ya Kiswahili ziliweza kuwasilishwa na kuchanganuliwa kwa njia ya michoroti.

**Uwasilishaji wa sentensi katizwa**

Katika utafiti huu, tuliwasilisha sentensi katizwa kwa njia ya matawi kwa mujibu wa nadharia ya sarufi miundo katizwa. Kwa mujibu wa Chomsky (1965), kanuni za sarufi miundo virai hutambulisha maumbo msingi ya sentensi. Kanuni hizi hutumia alama kama vile;

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

S Sentensi

N Nomino

T Kitenzi

V Kivumishi

E Kielezi

W Kiwakilishi

U Kiunganishi

HU Kihusishi

HI Kihisishi

Alama hizi za aina ya maneno huweza kutumiwa kujenga virai ambavyo vinaweza kuwakilishwa katika alama zifuatazo;

KN Kirai nomino

KT Kirai kitenzi

KV Kirai kivumishi


KE Kirai kielezi

KH Kirai kihusishi

Nadharia ya Harman (1963) imekuza na kupanua matumizi ya sheria hizi katika isimu kupitia mchakato wa ukatizwaji kwenye sentensi katizwa.

**Uchanganuzi wa sentensi katizwa**

Sentensi katizwa zilichanganuliwa kulingana na nadharia ya sarufi miundo katizwa kwa kuzingatia dhana ya mchoroti katizwa. Mfano ni; 'Juma alizungumza, bila shaka, kuhusu siasa.' Mfano huu uliweza kuchanganuliwa kwa kutumia mchoroti katizwa.





Kutokana na mchoroti huu katizwa, kirai 'bila shaka' kimeingia ndani ya sentensi hii na kukatiza mfululizo uliokuwepo ambao ni 'Juma alizungumza kuhusu siasa.' Ukatizwaji umetokea wakati kirai "bila shaka" kimeingilia kati kwa namna ambayo uhusiano wa moja kwa moja hauwezi kudhihirika kati ya vipashio hivi bila ya kuwepo na mistari ya ukingamo katika mchoroti huo.

Mfano mwingine wa sentensi katizwa ni; Siku njema, kwa hakika, huonekana asubuhi.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355




Katika sentensi katizwa; Siku njema, kwa hakika, huonekana asubuhi, kirai kihusishi kimetumiwa kama kielezi na kuchopekwa ndani ya sentensi hii ili kukatiza mfululizo wake. Ni wazi kwamba ikiwa kiambajengo kimetengwa kutoka kwa kichwa chake na elementi inayotawala kichwa chake, basi ukatizwaji huwa umetokea. Kwa hivyo, ni wazi kwamba mchoroti huu unawakilisha ukatizwaji.

Sentensi hii inaweza ikachanganuliwa kwa njia tofauti kwa kuzingatia dhana ya mfululizo wa mfuatano wa kupakana kwa kutoa maelezo ya jumla kuhusu dhana ya jozi inayopakana au ujirani wa kushoto na kulia kama inavyotokea katika miundo yenye ukatizwaji kama iyobainishwa;

S ⟶ N+V+ {KH} +T+KE ambapo mabano ya mraba yanaonesha kwamba KH hakitawaliwi na S, bali ni muktadha wa ndani tu huku alama hasi ikidhihirisha mfuatano wa kupakana wa vipashio.

Kulingana na utafiti huu, ni bayana kwamba sentensi zifuatazo katizwa zinaweza pia zikachanganuliwa kwa njia ya mchoroti;

5. Ukitaka kupata kitu bwana, **hebu nyamaza wee mtoto**, sharti ukihangaikie.

6. Uzuri wa suala hili, **unafahamu,** ni kufuatilia hadi mwisho.

7. Basi nilipofika nyumbani, **unasikia sana bwana**, nikamkuta tayari kapumzika.

8. Mbuzi, **aliyenunuliwa juzi**, amechinjwa leo asubuhi.

9. Barua ilitumwa, **samahani**, haikumfikia Shakila.

10. Mtoto **uliyemwona juzi** anasoma darasa la tano.

11. Sabiba, **mmojawapo ya wanawake wajawazito**, amejifungua mtoto wa kike.


Katika sentensi hizi tulitambua kwamba maneno yaliyoandikwa kwa rangi iliyokolea yamechopekwa kukatiza mwendelezo wa sentensi kuu kwa madhumuni maalumu.

**Mfano wa sentensi;** Shati hili, ingawa nalichukia, nitalivaa leo jioni.

Tuliweza kuwakilisha mfano huu kwa njia hii;

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355




Tungo ya maneno, 'ingawa nalichukia,' imeingizwa katika sentensi hii kukatiza mfululizo wake ingawa vinahitajika kuwa pamoja ili kukamilisha maana iliyokusudiwa. Katika utafiti huu, tulibaini ya kwamba ikiwa kiambajengo kinatengwa kutoka kwa kichwa chake na elementi inayotawala kichwa chake basi ukatizwaji unatokea. Mifano mingine ya sentensi katizwa ni;

12. Mtu huyu, **nina hakika,** alikuwa jasusi.
13. Vitabu **vilivyookotwa kwenye barabara ya kwenda Tanga** vimechapishwa.
14. Tumemwomba mwalimu**, kwamba**, aje kufundisha kesho.
15. Wapinzani walizungumza, **kwa kawaida**, juu ya siasa.
16. Watu wengi waliamini, **nipe nauli**, ijapokuwa walisaliti.

## HITIMISHO

Makala hii ilikusudia kushughulikia uchanganuzi wa viambajengo katizwa katika kiwango cha virai na sentensi. Masuala muhimu yaliyoangaziwa katika makala hii ni; uchanganuzi wa sentensi katizwa na virai katizwa katika lugha ya Kiswahili kwa matumizi ya michoroti katizwa, urahisishaji wa sentensi katika lugha, utambuzi wa dhima ya maneno katika tungo na ukuzaji wa matumizi ya istilahi za isimu ya Kiswahili ambazo msingi wake ni sarufi miundo virai katizwa. Pia, matokeo katika makala hii yameonyeshakuwa ikiwa kiambajengo kinatengwa kutoka kwa kichwa chake na elementi inayotawala kichwa chake basi ukatizwaji unatokea. Imebainika kuwa vipashio vichache visivyofululiza katika lugha bado hukubalika na kutoa maana na kwa kuwa Kiswahili ni lugha yenye muundo wa maneno usiobadilika, umeruhusu sentensi chache ambazo ni katizwa. Utafiti huu umeweza kubaini aina ya ukatizwaji na muktadha unaoruhusu viambajengo katizwa kuwa sahihi kisarufi katika lugha ya Kiswahili kwa kuzingatia nadharia ya sarufi miundo virai katizwa. Makala hii inapendekeza kufanyika kwa tafiti zaidi za kiisimu katika aina nyingine ya kirai kama kirai kihusishi, kirai kivumishi kwa kuzingatia nadharia nyinginezo ili kuzalisha maarifa Zaidi.

## MAREJELEO


Bloomfield, L. (1933*). Language*. New York: Holt, Rinehart &Winston.

Chomsky, N. (1965). *Aspects of the Theory of Syntax*. MA: MIT Press.

Habwe, J. & Karanja, P. (2004). *Misingi ya Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers.

Harman, G. (1963). Generative Grammars without Transformaton Rules: *A Defense of Phrase Structure*. Language 39, pg. 597-626.

Lincoln, Y. S., & Guba, E. G. (1985). *Naturalistic inquiry*. Newbury Park, CA: Sage.

Manaster-Ramer, A. & Kac, M. B. (1990). The Concept of Phrase Structure. *Linguistics and Philosophy, Jun., 1990, Vol. 13, No. 3 (Jun.,*

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.2355

*1990), pp. 325- 362*. https://www.jstor.org/stable/25001390

Massamba, D. P. (2004). *Kamusi ya Isimu na Falsafa ya Lugha*. TUKI: Dar es Salaam.

Milroy, A. L. (1987). *Observing and Analysing Natural Languages*. Oxford: Bas Blackwell Ltd.

Poole, G. (2002). *Syntactic Theory*. New York: Palgrave.

Reinholtz, C. (1999). On Characterization of Discontinuous Constituents: Evidence from Swampy Cree. *International Journal of American Lingustics*, 65(2), pg 201-227. https://www.jstor.org/stable.

Rubanza, C. (2003). *Basic Reading*. Dar es Salaam: Macmillan Aidan Ltd.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.